# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO

**MHESHIMIWA DKT. JUMA MALIK AKIL (MBM)**

## AKIWASILISHA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2026 NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA 2026/2027

**JUNI, 2026**

## YALIYOMO


A. UTANGULIZI .......... 1
B. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2025 .......... 4
Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia .......... 5
Mfumuko wa Bei Duniani .......... 6
Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar .......... 7
HALI YA AJIRA .......... 9
SEKTA YA UTALII .......... 10
Uingiaji wa Watalii .......... 10
C. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2025/2026 KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2025 HADI MACHI 2026) .......... 15
D. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2026 .......... 27
E. MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/2027 .......... 32
F. Mapendekezo ya Maeneo ya Kimkakati kwa Mwaka 2026/ 2027 .......... 33
Rasilimali kwa Ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2026/2027 .......... 34
G. MAENEO MTAMBUKA .......... 35
Masuala ya Idadi ya Watu .......... 35
Uhifadhi wa Mazingira .......... 36
Makundi yenye Mahitaji Maalum .......... 37
Kudhibiti Madawa ya Kulevya .......... 38
Mipango ya Kuendeleza Watenda Kazi .......... 39
H. UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI .......... 40
I. MAJUMUISHO .......... 40
J.HITIMISHO .......... 43

## A. UTANGULIZI

**1.0 Mheshimiwa Spika.** Kwa kuzingatia Kanuni ya 106 (2) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Agosti 2024, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee na kujadili na kushauri **Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2026/2027** unaojumuisha Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2025 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) kwa mwaka 2025/2026 pamoja na Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar 2026 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/2027. Hotuba hii ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2026/2027 ninayoiwasilisha leo inaambatana na Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2025 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) pamoja na Kitabu cha Pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2026 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2026/2027.

**2.0 Mheshimiwa Spika,** Utayarishaji wa Hotuba hii na taarifa za vitabu hivyo, vimezingatia kufikia Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Mipango ya Taifa ya muda wa Kati ikiwemo Mapitio ya Mpango wa muda wa kati (ZADEP) 2021/2026, Ilani ya uchaguzi ya chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025-2030, Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa wakati wa **Ufunguzi wa Baraza la Kumi na Moja (11) la Wawakilishi** na ahadi anazozitoa anapokutana na wananchi katika nyakati tofauti. Vile vile, mazingatio ya mpango huu yapo katika makubaliano ya Kikanda na ya Kimataifa yakiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya mwaka 2015 – 2030; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 1963; Ajenda ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2050; pamoja na Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya Mwaka 2050. Aidha, Mpango umekwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na teknolojia yanayoendelea duniani. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Programu

na Miradi ya Maendeleo kisekta ni moja ya nyenzo zilizotumika kujua utekelezaji halisi wa Mipango ya Maendeleo kwa kubainisha mafanikio na changamoto.

**3.0 Mheshimiwa Spika,** Shukurani za pekee ziende kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema iliyoniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako kwa mara nyengine kuwasilisha **Hotuba ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2026/2027.** Ninamshukuru Mola kwa kulijaalia Taifa letu amani, utulivu na mshikamano na kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa Baraza la 11 la Wawakilisha ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya Taifa kupitia Bajeti zilizowasilishwa katika Mkutano huu wa kujadili Bajeti. Napenda kuwashukuru wananchi wa Zanzibar kwa kufanikisha uchaguzi wa mwaka 2025 kwa amani na utulivu na kupelekea Chama cha Mapinduzi kupata ushindi wa kishindo wa nafasi ya Uraisi, Wabunge pamoja na Wawakilishi kupitia majimbo mbali mbali Unguja na Pemba.

**4.0 Mheshimiwa Spika,** Pongezi na shukrani za kipekee zimwendee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa DKt. Hussein Ali Mwinyi kwa kushika usukani kwa mara ya pili katika Awamu ya Nane na kuiongoza tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa umahiri mkubwa. Uongozi wake umeonesha dhamira ya dhati ya kuendeleza hali ya amani na utulivu iliyopo nchini pamoja na kuinua Uchumi wa Zanzibar. Vile vile naomba pia nitoe pongezi za dhati kwa Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa tena kuwa Makoamo wa Pili wa Raisi ambae ndio msaidizi mkuu wa Mheshimiwa Rais. Juhudi zako zinasaidia kukuza na kuimarisha ustawi wa nchi na wananchi kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape viongozi hawa umri mrefu, afya njema na uongozi wenye uadilifu kwa kipindi chote cha kutuongoza na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**5.0 Mheshimiwa Spika,** Nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

aliyeshika wadhifa huo kwa ushindi mkubwa kutoka kwa watanzania waliojenga imani kwake kutokana na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yake pamoja na kulilinda Taifa la Tanzania dhidi ya wasioitakia mema nchi yetu. Kwa hakika Dkt. Samia anaendelea kuweka historia kubwa Barani Afrika ya kuwa mwanamke wa kwanza Afrika Mashariki kushika nafasi ya urais na kuweza kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuliletea Taifa na wananchi maendeleo makubwa. Vile vile, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6.0 **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa napenda nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na viongozi wa Baraza hili Tukufu. Shukrani za kipekee ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wote wa kamati ya Bajeti kwa mashirikiano makubwa na miongozo iliyopelekea hadi leo nasimama hapa kuwasilisha hotuba hii. Naamini, kwa juhudi kubwa na maarifa mnayonipatia nitaweza kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu na ufanisi zaidi na kukidhi kiu ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

7.0 **Mheshimiwa Spika,** Wakati dunia ikiendelea na mbinu mbali mbali za kujenga Uchumi wake, mgogoro wa vita uliotokea baina Marekani-Israel dhidi ya Irani unarudisha nyuma jitihada hizo. Maelfu ya wananchi wamepoteza maisha yao na chumi za nchi mbali mbali zinahofiwa kutetereka kutokana na kuathirika kwa baadhi ya shughuli kuu za Uchumi zikiwemo sekta ya utalii, usafirishaji, uwekezaji mitaji na biashara sambamba na kupanda kwa bei za mafuta ambazo zinaathiri uzalishaji wa ndani na uchumi wa dunia. Zanzibar na Tanzania kwa ujumla inaendelea na jitihada za kufuatilia kwa makini ili kupunguza madhara ya vita hiyo kwa nchi yetu. Mola awape nuru viongozi wa mataifa yaliyoingia katika machafuko hayo kuweza kupata maarifa zaidi na mioyo ya imani ya kutokomeza vita hiyo ili kuwanusuru wananchi wasio na hatia pamoja na dunia kwa ujumla.

**8.0 Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2026/2027 ni mpango wa mwanzo katika utekelezaji wa mipango ya muda wa kati ya kipindi cha pili cha awamu ya nane ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi. Mipango hiyo ni pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025-2030, Hotuba ya ufunguzi wa Baraza la 11 la Wawakilishi na Mapitio ya Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026. Mpango huu utazingatia pia Maelekezo ya Serikali Kiujumla, ahadi zilizotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi pamoja na maagizo kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika mikutano mbali mbali.

**9.0 Mheshimiwa Spika,** Matarajio ni kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, kuifikisha Zanzibar kuwa nchi yenye hadhi ya kiwango cha juu cha Uchumi wa Kipato cha Kati (Upper Middle-Income Status) ifikapo mwaka 2050, kwa kuwa na sifa zifuatazo: Maisha bora, amani, utulivu na umoja; utawala na uongozi imara; jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi; uchumi wenye uwezo wa kuhimili ushindani; na ukuaji endelevu kwa maslahi ya watu wote.

**10.0 Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha muhutasari wa Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2025 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) pamoja na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2026 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2026/2027.

## B. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2025

**11.0 Mheshimiwa Spika,** Mapitio haya yametokana na uchambuzi wa viashiria vya uchumi jumuishi ambavyo ni muhimu katika kupanga maendeleo ya Taifa. Uchambuzi wa viashiria vya uchumi vimeweka misingi imara iliyotumika kuandaa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027. Viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni pamoja na: Pato la Taifa; Mfumuko wa bei; mwenendo wa Sekta ya nje; Sekta ya fedha;

Deni la Serikali; na viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo idadi ya watu na hali ya umaskini nchini.

**Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia**

**12.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia (World Economic Outlook, April 2026). Inaonesha kuwa kwa mwaka 2025, uchumi wa dunia umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.4 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa huduma za kifedha na kuongezeka kwa uwekezaji unaohusiana na teknolojia ikiwemo ya akili mnemba (AI), hasa katika maeneo ya nchi za Amerika Kaskazini na Asia pamoja na kuimarika kwa masoko ya hisa kwa nchi zilizoendelea na kupelekea kuongezeka upatikanaji wa mitaji kwa kampuni za uwekezaji na kuongeza kasi ya ukuaji uchumi katika Nchi zinazoendelea. Taswira ya ukuaji wa uchumi wa dunia imegawika katika makundi tofauti kama ifuatavyo:-

i. **Uchumi kwa Nchi Zilizoendelea:** Ukuaji umefikia wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 1.7 kwa mwaka 2024, ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa biashara za Kimataifa na kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji;

ii. **Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi:** Ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa thamani ya masoko ya fedha na mitaji na kukua kwa biashara za usafirishaji wa bidhaa za viwandani zenye umiliki na uwakala kutoka katika Kampuni za Marekani na Ulaya;

iii. **Uchumi wa Nchi za Afrika:** Kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2025 kutoka ukuaji kama huu mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa umma, kuongezeka kwa matumizi ya sekta binafsi pamoja na maboresho makubwa ya kiuchumi yaliyofanyika katika ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na kuimarika kwa mifumo ya

teknolojia ya huduma ya fedha katika nchi za Nigeria, Senegal na Ghana;

iv. **Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki:** Kasi ya Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki umefikia wastani wa asilimia 5.7 kutoka asilimia 5.1 iliyorekodiwa mwaka 2024. Hii imetokana na kuimarika kwa uwekezaji wa umma, viwanda na huduma kwa nchi ya Uganda, kuimarika kwa miradi ya miundombinu, utalii pamoja na kuimarika kwa sekta ya uchimbaji madini na gesi asilia kwa Tanzania, kuimarika kwa sekta ya kilimo, ujenzi na huduma kwa nchi ya Kenya na kuimarika viwanda kwa nchi ya Ruwanda; na

v. **Kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (Sub Saharan Countries):** Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2025 imefikia wastani wa asilimia 4.5 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2024. Kuimarika kwa uchumi katika nchi za eneo hili, kumetokana na uwekezaji wa miradi mikubwa ikiwemo miradi ya nishati ya umeme na teknolojia ya huduma za kifedha na benki, ambapo kumeshajihisha zaidi wawekezaji binafsi kuekeza katika miradi ya maendeleo.

## Mfumuko wa Bei Duniani

**13.0 Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa mwenendo wa kasi ya mfumuko wa bei duniani ni muhimu sana katika kubuni sera na mikakati ya kudhibiti athari za kupanda kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. Kama tunavyofahamu kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei za bidhaa na huduma huongeza thamani na kupunguza nguvu ya usawa katika ununuzi. Kasi ya mfumuko wa bei duniani imefikia asilimia 4.1 kutoka asilimia 5.8 ya mwaka 2024. Hii imetokana na kupungua kwa bei za bidhaa, viwango vya riba na udhibiti wa sera za kifedha. Mfumuko wa bei una sura tofauti kwa maeneo mengine duniani kama ifuatavyo:

i. Kasi ya mfumuko wa bei kwa **Nchi Zilizoendelea** imepunguwa kwa wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2024. Hii ni kutokana na Benki Kuu ya

**Marekani (U.S. Federal Reserve) na Benki Kuu ya Ulaya (European Central Bank)** kudhibiti mfumuko wa bei kwa kuongeza viwango vya riba kuwa juu na kudhibiti kiwango cha fedha kwenye uchumi na kupelekea kupunguza matumizi kupita kiasi kwa ajili ya kupunguza kasi ya kupanda kwa bei;

ii. **Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi** zimefikia wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2024. Kupungua kwa mfumuko wa bei kumetokana na kupungua kwa bei za chakula kwa nchi ya China pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa za nishati kwa nchi ya Dubai;

iii. **Kasi ya mfumuko wa bei katika ukanda wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara** imepungua na kufikia wastani wa asilimia 12.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 20.7 mwaka 2024; na

iv. **Kasi ya Mfumuko wa bei kwa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki** imepungua na kufikia wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 10.6 mwaka 2023. Upungufu huo ni kutokana na Benki Kuu katika nchi kama Tanzania, Kenya na Uganda kutekeleza sera za kifedha kwa kudhibiti kiwango cha fedha na viwango vya riba, kupungua kwa bei za nishati zilizopelekea kupunguza gharama za usafirishaji na uzalishaji pamoja na mavuno mazuri katika nchi kadhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar

**14.0 Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2025/2026 unategemea sana mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi kama ndio msingi wa mwelekeo wa Mipango ya nchi. Baadhi ya viashiria hivyo ni pamoja na ukuaji wa uchumi, mfumko wa bei, mwenendo wa sekta ya nje, uingiaji wa watalii na uwekezaji.

**15.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025 uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika ambapo kwa mujibu wa viashiria vya kiuchumi, Pato Halisi la Taifa (GDP at Constant Price) limeongezeka

na kufikia thamani ya TZS 4,307.9 bilioni kutoka thamani ya TZS 4,026.4 bilioni mwaka 2024 sawa na kasi ya ukuaji wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2024. Aidha, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at Current Price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 7,029.9 bilioni kutoka thamani ya TZS 6,572.6 bilioni mwaka 2024. Ukuaji huo wa asilimia 7.0 ulichangiwa na:

i. Kuimarika kwa sekta ya kodi za bidhaa, ambapo kwa mwaka 2025 imekuwa kwa wastani wa asilimia 12.8 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2024;

ii. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii nchini wapatao 917,167 mwaka 2025 kutoka watalii 736,755 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 24.5;

iii. Kuongezeka kwa miradi mipya ya uwekezaji kwa asilimia 3.8 kufikia miradi 136 yenye thamani ya TZS 1,894,078 milioni iliyosajiliwa mwaka 2025 kutoka miradi 131 yenye thamani ya TZS 1,877,760 milioni iliyosajiliwa mwaka 2024; na

iv. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia TZS 1,615.8 bilioni julai-machi mwaka 2025/26 ikilinganishwa na jumla ya TZS 1,299.0 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 24.3.

**16.0 Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu zilizopelekea kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi mwaka 2025 ikilinganishwa na mwaka 2024 ni kutokana na:

i. Kupungua kwa mchango wa sekta ya kilimo ambayo inajumuisha sekta ndogo ya Mazao, Ufugaji, Misitu na Uvuvi kufikia asilimia 23.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 24.3 mwaka 2024; na

ii. Kupungua kwa ukuaji wa sekta ya viwanda ambayo inajumuisha sekta ndogo ya uchimbaji mawe na mchanga, ujenzi, umeme na gesi, utengenezaji wa bidhaa za viwandani na shughuli za usambazaji maji na maji taka kufikia asilimia 19.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 20.2 mwaka 2024.

**Pato la Mwananchi**

**17.0 Mheshimiwa Spika**, Kuongezeka kwa Pato la Taifa kumepelekea kuongezeka kwa kipato cha mwananchi. Kwa mwaka 2025 Pato la Mwananchi Zanzibar limeongezeka na kufikia TZS 3,349 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,320 kutoka TZS 3,227 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,243 mwaka 2024. Zanzibar inakadiriwa kufikia idadi ya watu 2,099.0 milioni mwaka 2025 kutoka watu 2,036.5 milioni walioripotiwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3.0 kwa makadirio ya mwaka.

**Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar**

**18.0 Mheshimiwa Spika**, Kasi ya mfumuko wa bei kwa mwaka 2025 imepungua na kufikia wastani wa asilimia 4.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024. Upungufu huo umesababishwa na kupungua kwa bei za bidhaa za chakula ambapo mfumuko wa bei umefikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 8.4 mwaka 2024. Aidha, kwa upande wa bidhaa zisizo za chakula kwa mwaka 2025 mfumuko wa bei umefikia wastani wa asilimia 3.4 ukilinganisha na wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2024.

**19.0 Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumuko wa bei Zanzibar ingeweza kuwa ya juu zaidi lakini Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu kwa wananchi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi. **Benki Kuu ya Tanzania (BoT)** inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kudhibiti sera za kifedha ikiwemo kushuka kwa thamani kwa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani.

**HALI YA AJIRA**

**20.0 Mheshimiwa Spika,** Kuimarika kwa shughuli za uzalishaji pamoja na hali ya amani na utulivu kumeongeza ajira rasmi na zisizo rasmi.

Kwa mwaka 2024/2025, jumla ya ajira mpya zilizosajiliwa kutoka Serikalini, Mashirika ya Serikali na Sekta Binafsi zimefikia ajira 85,182 (wanaume ni 42,760 na wanawake ni 42,422) ikilinganishwa na ajira 83,430 (wanaume ni 43,629 na wanawake ni 39,801) ambazo zilisajiliwa mwaka 2023/2024. Ajira zilizotolewa na Sekta binafsi katika kipindi hichi zimefikia 34,506 na za Mashirika ya Serikali ni 9,299. Kwa upande wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa mwaka 2025 jumla ya ajira zilizopatikana kwa miradi mipya ni 6,494 kutoka ajira 4,109 zilizosajiliwa mwaka 2024 miradi iliyotoa ajira nyingi zaidi kuliko miradi mengine ni miradi ya huduma za hoteli na migahawa kufikia ajira mpya 3,888 ikifuatiwa na miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara (Real Estate) kufikia ajira mpya 1,527.

## SEKTA YA UTALII

### Uingiaji wa Watalii

**21.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha sekta ya utalii ikiwa ni kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar inayochangia zaidi ya asilimia 30 ya Pato la Taifa. Kwa mwaka 2025 idadi ya watalii imeongezeka kwa asilimia 24.5 kufikia watalii 917,167 ikilinganishwa na watalii 736,655 waliorikodiwa mwaka 2024. Ongezeko hili limepelekea kuongezeka kwa thamani ya mauzo yatokanayo na uhaulishaji wa huduma (Receipts from Service Account) yenye jumla ya Dola za Kimarekani 1,409.4 milioni kwa mwaka ulioishia Disemba 2025, kutoka dola za Kimarekani 1,126.4 milioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 25.1 na kuongezeka kwa wastani wa siku za kutalii *(Average days of stay)* kufikia siku 7 kutoka siku 6 mwaka 2024. Jitihada zilizochukuliwa na Serikali pamoja na Sekta Binafsi ni:

i. Kuitangaza Zanzibar kimataifa na ziara za Viongozi Wakuu, Mawakala wa usafirishaji watalii pamoja na Mabalozi wetu wa Tanzania nje ya nchi;

ii. Kuimarika kwa uwekezaji nchini na masoko ya utalii duniani;

iii. Kuimarika kwa miundombinu ya usafirshaji, huduma za kitalii nchini zikiwemo hoteli za nyota tano sambamba na huduma zinazotolewa;

iv. Kuendelea kushiriki katika makongamano ya kibiashara na uwekezaji katika mataifa mbali mbali duniani;

v. kuendelea kuitangaza Zanzibar kiutalii; kupitia Wana Diplomasia wa Tanzania

vi. Kuhamasisha masoko mapya ya utalii na kuleta ndege za moja kwa moja (Direct Flights) kuja Zanzibar; na

vii. Kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**MWENENDO WA THAMANI YA SHILINGI YA TANZANIA DHIDI YA DOLA YA MAREKANI**

**22.0 Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani ni muhimu kutokana na mauzo na ununuzi wa bidhaa nje ya nchi. Kwa mwaka 2025 fedha ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,538 kwa Dola moja ya kimarekani ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,597.0 kwa mwaka 2024. Sawa na ongezeko la thamani kwa wastani wa asilimia 2.2. Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti sarafu ya Tanzania katika hali ya utulivu kwa kuongeza mzunguko wa fedha (Money circulation), kupitia usafirishaji wa madini ya dhahabu na bidhaa za chakula.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

**23.0 Mheshimiwa Spika,** Fedha za kigeni zinaendelea kuhifadhiwa (Foreign reserve) ili kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2024/25, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani 6.2 bilioni ikilinganishwa na dola za Marekani 5.3 bilioni kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4 na siku 8. Kiasi hicho ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha

za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua minne.

## SEKTA YA NJE

### Urari wa Biashara

**24.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025, nakisi ya biashara imefikia thamani ya TZS 2.4 trilioni kutoka thamani ya TZS 1.4 trilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 63.3, hali iliyosababishwa na ongezeko kubwa la thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje kuliko Usafirishaji wa bidhaa kwenda nje. **Thamani ya Uagiziaji** wa bidhaa kutoka nje ya nchi imefikia TZS 2.4 trilioni kutoka thamani ya TZS 1.6 trilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 50.0. Bidhaa zilizoingia nchini ni bidhaa za vyakula, nishati ya mafuta, bidhaa za mashine, vifaa vya viwandani, zana za kilimo, mali ghafi za viwandani, nguo na mapambo, bidhaa za samani, vifaa vya ujenzi, Afisini na nyenginezo.

**25.0 Mheshimiwa Spika,** Usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi umefikia thamani ya TZS 92.4 bilioni kutoka thamani ya TZS 105.2 bilioni ya mwaka uliopita sawa na upungufu wa asilimia 12.0. Upungufu huo umechangiwa na kupungua kwa thamani ya usafirishaji wa bidhaa za baharini kufikia thamani ya TZS 35.5 bilioni mwaka 2025 kutoka thamani ya TZS 36.1 bilioni mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 2.0. Upungufu huo umechangiwa na upatikanaji mdogo wa samaki aina ya dagaa mwaka 2025 kufikia tani 18,318 kutoka tani 18,678 mwaka 2024 sawa na upungufu wa tani 360.

**26.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025, **usafirishaji wa zao la karafuu** umefikia jumla ya tani 3,186.1 zenye thamani ya TZS 52.8 bilioni kutoka tani 1,974.4 zenye thamani ya TZS 30.7 bilioni zilizosafirishwa mwaka 2024. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa uzalishaji wa zao la karafuu kufikia tani 5,230.4 mwaka 2025 kutoka tani 1,167.4 mwaka 2024 zilizonunuliwa na **ZSTC** kutoka kwa wakulima nchini.

**27.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025, Serikali imeendelea na usafirishaji wa mazao ya baharini ikiwemo dagaa kavu, mwani, majongoo bahari, kaa na mazao mengineo. Kwa upande wa dagaa kavu usafirishaji umefikia jumla ya tani 6,035 zenye thamani ya TZS 27.9 bilioni mwaka 2025 kutoka tani 5,466.62 zenye thamani ya TZS 24.5 bilioni mwaka 2024. Zao la mwani limefikia jumla ya tani 3,901.8 zenye thamani ya TZS 5.2 bilioni mwaka 2025 kutoka tani 7,089.5 zenye thamani ya TZS 10.7 bilioni mwaka 2024.

**Mwenendo wa Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Intra trade)**

**28.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umefikia thamani ya TZS 155.3 bilioni kutoka thamani ya TZS 280.8 bilioni mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 45.0. Kutokuwepo kwa uhitaji wa bidhaa zinazosafirishwa kwenda Tanzania bara (re-exported goods) kumechangia kupunguza uhaulishaji mwaka 2025. Kwa upande wa uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umefikia thamani ya TZS 668.6 bilioni mwaka 2025 kutoka thamani ya TZS 549.6 bilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 22.0. Bidhaa zinazohaulishwa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ni mchele wa mbeya, mchele wa basmati, mafuta ya kula, vitunguu, tungule, mkaa, mayai, matunda na mengineyo.

**29.0 Mheshimiwa Spika,** Kuongezeka kwa thamani ya mauzo yatokanayo na uhaulishaji wa huduma hasa za utalii nje ya nchi pamoja na usafirishaji wa karafuu na mwani, kumepelekea ziada ya Account ya uhaulishaji wa huduma, usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa (Current Account Surplus) kwa asilimia 34.0 na kufikia thamani ya Dola za Kimarekani 943.3 milioni kutoka thamani ya Dola za Kimarekani 704.1 milioni mwaka 2024

### Ukuzaji Rasilimali

**30.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imesajili jumla ya miradi 136 yenye thamani ya TZS 1,894.0 bilioni kutoka miradi 131 yenye thamani ya TZS 1,877.7 bilioni mwaka 2024 sawa na asilimia 0.86 ya thamani ya miradi hiyo. Miradi yenye thamani kubwa zaidi iliyowekezwa nchini ni miradi ya nyumba za biashara/mali zisizohamishika (Real Estate) yenye thamani ya TZS 803.2 bilioni ikifuatiwa na miradi ya hoteli na migahawa (Huduma za Malazi na Chakula) yenye thamani ya TZS 726.6 bilioni.

### Mikopo wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

**31.0 Mheshimiwa Spika,** Wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2025/26 wameongezeka kufikia wanafunzi 8,957 kutoka wanafunzi 4,629 kwa mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 93. Hii inatokana na kuongezeka kwa ufaulu pamoja na Serikali kufungua dirisha kwa wanafunzi wa ngazi ya Stashahada. Aidha, Serikali imeongeza fungu la mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kufikia TZS 35 bilioni kwa mwaka 2025/26 kutoka TZS 30.5 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Hadi kufikia Machi 2026, TZS 4.3 bilioni zimekusanywa kama marejesho ya mikopo ya elimu ya juu sawa na asilimia 75.4 ya shabaha ya TZS 5.7 bilioni.

## UTEKELEZAJI WA ZANZIBAR SUKUKI

**32.0 Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kuimarisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya Maendeleo, Serikali kupitia Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/25 ilianzisha mfumo mbadala wa uwekezaji unaozingatia misingi ya Sheria (Sheria za Kiislam) unaojulikana kama Sukuk. Hatua hii imepanua wigo wa vyanzo vya fedha na kufungua milango kwa wawekezaji mbalimbali kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi imara unaozingatia maadili ya Kiislam na uwazi.

**33.0 Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2026, Serikali imeshatenga jumla ya TZS 49.61 bilioni na USD 17.33 milioni kwa

ajili ya kurejesha mtaji pamoja na kugharamia faida kwa wawekezaji wa Sukuk. Kati ya hizo, jumla ya TZS 17.28 bilioni na USD 3.39 milioni zimelipwa kama sehemu ya gawio la faida ambapo faida ya awali ya nusu mwaka ya kwanza ililipwa tarehe 22 Oktoba, 2025 yenye jumla ya TZS 8.64 bilioni na USD 1.69 milioni. Aidha, Serikali inatarajia kukamilisha malipo ya nusu ya pili ya mwaka wa kwanza tarehe 22 Aprili 2026 kwa kiwango sawa cha TZS 8,64 bilioni na USD 1.69 milioni. Hivyo, jumla ya fedha iliyobaki kwa ajili ya kulipa mitaji ambayo imewekezwa kwenye benki mbali mbali zinazofuata misingi ya Sharia ni TZS 32.33 bilioni na USD 13.93 milioni.

**34.0 Mheshimiwa Spika,** Kupitia uwekezaji huu, miradi mbalimbali ya kimkakati imetekelezwa, ikiwemo ujenzi wa uwanja wa Ndege Unguja Terminal 2, uimarishaji wa miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba, maendeleo jumuishi ya Bandari ya Mangapwani na masoko ya samaki ya kisasa (Mkoani na Fungurefu).

**35.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla, Sukuk imejidhihirisha kuwa ni ufunguo wa soko la kifedha linalofuata Misingi ya Sharia pekee na daraja linalounganisha ndoto za maendeleo na uhalisia wake.

## C. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2025/2026 KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2025 HADI MACHI 2026)

**1.0 Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026 ni mpango wa tano wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Mpango huo ulipanga kutekeleza programu 41 na miradi 56 ya maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 4,539.64 bilioni kwa kutekeleza shughuli za maendeleo ambapo kiasi cha TZS 3,231.40 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1,308.24 bilioni zilipangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (TZS 962.74 bilioni ni mikopo na TZS 345.50 bilioni ni ruzuku).

**2.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, matumizi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yamefikia jumla ya TZS 1,769.27 bilioni sawa na asilimia 65 ya lengo la TZS 2,723.83 bilioni kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo TZS 1,414.53 bilioni ni kutoka Serikalini na TZS 354.74 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Utekelezaji wa Maeneo ya Kimkakati kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai 2025 – Machi 2026)**

**3.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipanga kutekeleza Programu na Miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi Matano (5) ambayo ni: **Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu; Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu; Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; na Utawala Bora na Uhimilivu** kama yalivyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo (ZADEP) 2021-2026.

**4.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) jumla ya TZS 1,965.43 bilioni zilipangwa kutumika ili kutekeleza Programu na Miradi ya kimkakati (TZS 1,446.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 518.83 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1,484.12 bilioni sawa na asilimia 76 ya lengo la TZS 1,965.43 bilioni (TZS 1,238.77 bilioni sawa na asilimia 86 ya lengo la TZS 1,446.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 245.35 bilioni sawa na asilimia 47 ya lengo la TZS 518.83 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepatikana. Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Kimkakati kwa maeneo mahsusi ni kama ifuatavyo:

**I. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu**

**5.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza Programu na Miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 428.1 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kiasi cha TZS 256.86 bilioni zilipangwa kutumika ambapo, jumla ya TZS 186.06 bilioni sawa na asilimia 72 ya lengo

zimepatikana. Utekelezaji wa programu na miradi katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

a) **Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria:** Programu hii ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kulinda, kuhifadhi na kutunza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae sambamba na kusimamia ukuzaji wa shughuli za utalii kwa kuongeza fursa za ajira, vivutio vya utalii na kuongeza Pato la Taifa. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi tisa (9) ni uandaaji wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika maeneo ya Mwera, Pete, Dunga, Kuumbi, Mwanampambe na Mvuleni; ukarabati wa maeneo ya mradi katika eneo la Ras Mkumbuu – Pemba na Mangapwani – Unguja kwa ujenzi wa duka, mgahawa, sehemu ya mapumziko, vyoo, upakaji wa rangi katika Afisi, uwekaji wa ngazi, ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bahari, uwekaji wa njia za kupita na sehemu ya maegesho ya vyombo vya moto, uwekaji wa miundombinu ya usambazaji maji na umeme, upandaji wa bustani pamoja na ukarabati wa majengo ya kihistoria.

b) **Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani:** Mradi huu una lengo la kujenga bandari jumuishi ya kisasa Mangapwani (Multipurpose Port) ambayo itajumuisha ujenzi wa gati ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta na ujenzi wa chelezo cha kukarabati meli. Katika kipindi cha miezi tisa (9) kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa msingi na uzungushaji wa uzio katika eneo la ujenzi. Aidha, uwekaji wa ardhi sawa umefanyika katika eneo la Bumbwini kwa ajili ya kutengeneza miguu (pile) ya kushikilia daraja la bandari. Kwa upande wa ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi pamoja na chelezo Mangapwani; kazi zilizofanyika ni uchunguzi wa udongo, upimaji wa kina cha maji, kufungwa kwa vifaa vya ujenzi vikiwemo *Flowmeter, manifold, buoys, pipe line na Platform.* Kazi za kuweka miundombinu ya bandari inaendelea.

c) **Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi:** Mradi huu una lengo la kujenga bandari ya kisasa ambayo itajumuisha ujenzi wa bandari ya abiria na mizigo. Hadi kufikia Machi 2026, kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa ghala, maduka, ujenzi wa gati (causes way), mizani ya kupimia mizigo ujenzi na ufungaji wa tishali (Barge) zenye uwezo wa kuhudumia meli nne kwa pamoja ujenzi wa ukuta wa fensi na ufukiaji wa eneo la bahari. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 87.

d) **Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya kuchakata na Kusarifu Samaki:** Mradi una lengo la kuimarisha mnyororo wa sekta ya uvuvi na uongezaji wa thamani wa bidhaa kupitia usindikaji wa kisasa pamoja na kujenga viwanda vitakavyoshughulikia ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa samaki kwa masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi unaendelea na ujenzi wa viwanda katika eneo la Fungurefu, Ndagoni na Kama. Hadi kufikia Machi 2026, Fungurefu ujenzi upo katika hatua ya msingi; Ndagoni upo katika hatua za umaliziaji wa kazi za ujenzi wa jengo la Afisi, jengo la kupakulia na kuoshea dagaa, vyoo, chumba cha baridi, majengo ya mkahawa, biashara na kubadilishia nguo. Aidha, jengo la kiwanda cha kukaushia dagaa limefikia hatua ya msingi na barabara imejengwa kwa kiwango cha fusi; na kiwanda cha Kama ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji wa majengo mbali mbali ikiwemo jengo la biashara, vyoo, jengo la kubadilishia nguo namba 1 na 2, majengo ya kupakulia, kuoshea na kuchemshia dagaa, nyumba za wajasiramali, nyumba za wateja, jengo la kuhifadhi kemikali pamoja na eneo la kuanikia dagaa. Aidha, ujenzi wa majengo ya viwanda vya kukaushia na kuchakata dagaa umefikia hatua ya msingi na barabara (mita 300) imejengwa kwa kiwango cha zege.

## II.Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

6.0 **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 1,078.92 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 720.85 bilioni zilipangwa kutumika hadi kufikia

Machi 2026, jumla ya TZS 719.61 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo la TZS 720.85 bilioni zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:

a) **Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu:** Programu hii ina lengo la kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari ili kuhuisha uchumi na uwekezaji. Kazi zilizotekelezwa kwa kipindi hiki cha mapitio ni pamoja na ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 39.8 kwa kiwango cha lami; km 11.33 zipo katika hatua mbali mbali za ujenzi ikiwemo uwekaji wa tabaka la kwanza na la pili; uchimbaji wa mitaro km 6.72; usafishaji wa km 7.2 katika Barabara ya Mfenesini – Mangapwani, km 10.73 Chanjamjawiri – Tundaua, pamoja na uchunguzi wa udongo kwa barabara ya Tunguu - Makunduchi (km 48), Kisauni - Fumba (km 12) na Chake Chake – Mkoani (43.5km).

b) **Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani:** Programu ina lengo la kujenga barabara za ndani na vijijini ili kuweza kuunganisha mitaa na maeneo mengine ikiwemo barabara kuu na kusaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba na kupendezesha miji na mitaa katika maeneo ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2026 kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara zenye jumla ya kilomita 68 (km 33.58 zimejengwa kwa kiwango cha lami na km 34 zimejengwa kwa kiwango cha fusi). Ujenzi wa barabara kilomita 163.22, unaendelea na jumla ya kilomita 14.16 zimejengwa kwa kiwango cha lami (Unguja ni km 8.85 na Pemba ni km 5.31). Aidha, ujenzi wa barabara kilomita 65.5 ujenzi huo unaendelea kwa hatua mbali mbali Unguja na Pemba, barabara ya Wete-Konde - Gando imejengwa kwa kiwango cha lami (km 18) na zilizobaki zinaendelea kujengwa kwa hatua mbali mbali za kifusi.

c) **Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini:** Programu hii ina lengo la kuimarisha haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara katika maeneo ya Mjini. Mradi unahusisha ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za Mjini na uimarishaji wa barabara

katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Hadi kufikia Machi 2026, ujenzi wa barabara za juu (flyover) katika mzunguko (Roundabout) wa Mwanakwerekwe umekamilika na mzunguko wa Amani umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Ujenzi wa chelezo kwa pande zote mbili za ujenzi unaendelea. Barabara ya Mkapa kilomita 5, Mombasa Soko la Mboga – Azania (km 1.3) na Kwa Kira-Kituo kipya cha Uwanja wa Ndege (km 1.03) na zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, hatua mbali mbali za ujenzi kwa baadhi ya barabara za Mjini zinaendelea zikiwemo Kinazini-Mtoni kilomita 0.86, Amani–Mikunguni-Biziredi (km 2.55) na Kariakoo – Mwanakwerekwe (km 3.71) zinatarajiwa kuanza baada ya kukamilika taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi.

d) **Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege:** Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya Kimataifa vitakavyoweza kupokea ndege aina ya "Code 4C". Programu itahusisha ujenzi wa viwanja vya ndege Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2026, Kwa upande wa Terminal II katika uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amaan (AAKIA) kazi ya kuezeka, 'skimming', kupaka rangi, ufungaji wa *'conveyer belt',* ujenzi wa *'immigration counter',* uwekaji wa nguzo za kuunganisha *'terminal building* II na Terminal building III' pamoja na kazi za umaliziaji (skimming, floor tiles na ceiling) zinaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 94. Kwa upande wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba, ujazaji wa kifusi umekamilika katika eneo la 'Terminal Building' na eneo la ndani ya Uwanja (Airside), ujenzi wa njia ya kurukia ndege (Runway) unaendelea na kuchimbwa kwa ajili ya kujazwa kifusi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 6.

e) **Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar:** Programu hii ina lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama katika maeneo ya mjini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2026, kazi ya ufanyaji wa tathmini ya maeneo yatakayoathirika

na ulipaji wa fidia inaendelea. Kupitia mradi wa uimarishaji wa miundombinu ya maji Zanzibar vifaa mbali mbali vimenunuliwa ikiwemo pampu 40 maalum, bomba za kusafirishia maji, vifaa vya maji pamoja na ujenzi wa hifadhi za 'hydrant'. Aidha, Matangi 12 ya kuhifadhia maji na ukarabati wa tangi la lita 250,000 la Kengeja umekamilika. Kwa upande wa uimarishaji miundombinu ya maji Kaskazini Unguja - Ujenzi wa matangi mawili - Kilindi, uchimbaji wa visima vitatu (Mahonda viwili (2) na Kiashange – Matemwe kimoja (1)), ujenzi na matengenezo ya vibanda 30 vya kuhifadhia mashine, ununuzi wa pampu 20 za nishati ya jua, ulazaji wa mabomba kwa urefu wa kilomita 7.798 - Machui umekamilika sambamba na ununuzi wa mita 10,000 za maji. Kazi ya uandaaji wa miongozo ya sekta ya maji na usafi wa mazingira katika Maeneo ya Mijini imekamilika.

f) **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar:** Programu hii ina lengo la kuwa na umeme wa kujitosheleza ikiwa ni nyenzo muhimu ya kuimarisha shughuli za kiuchumi, usafiri na huduma za jamii kwa maeneo yote Mjini na Vijijini. Kupitia Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Serikali imeweza kusambaza umeme katika vijiji 63 (35 Unguja na 28 Pemba), nguzo 1,776 zimenunuliwa na nguzo 1,676 zimebadilishwa (1,155 Unguja na 521 Pemba), wateja wapya 38,800 (23,200 Unguja na 15,200 Pemba) kati ya wateja 43,000 wameunganishwa umeme, uvutaji wa njia mpya za umeme umefanyika na jumla ya wateja wapya 2,650 kati ya 2,500 sawa na asilimia 106 wameunganishwa (Pemba ni 825 na Unguja ni 1,825). Hadi kufikia Machi 2026, kazi zilizofanyika kwa Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar ni Ufungaji wa *"Voltage regulators Capacitor Bank"*, katika maeneo 26 na zoezi la usanikishaji wa STATCOM limekamilika kwa asilimia 100. Shughuli za uhamishaji wa wananchi katika maeneo ya Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko ya Sekta ya Nishati zinaendelea baada ya kukamilika zoezi la ulipaji wa fidia kwa waathirika 1,450 kati ya 1,510. Ujenzi wa vituo vya kupokelea na kusambazia umeme (Sub-Station) pamoja na uwekaji wa nguzo za umeme unaendelea

kwa maeneo ya Welezo, Ubago, Makunduchi na Matemwe. Aidha, uchimbaji wa misingi kwa ajili ya nguzo za umeme, ujenzi wa kuta na majengo ya uendeshaji, usimikaji wa vyuma na uwekaji wa nyaya za umeme kwa ajili ya ujenzi wa laini kubwa ya umeme yenye uwezo wa kilovoti 132 unaendelea na kazi ya uwekaji wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya umeme Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa vituo vya umeme kwa ajili ya ufungaji wa mitambo.

### III. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

7.0 **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa Kutekeleza Programu na Miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 148.9 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), jumla ya TZS 89.35 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 25.04 bilioni sawa na asilimia 28 ya lengo la TZS 89.35 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

a) **Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar:** Programu hii ina lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati katika maeneo ya Dimani na Chamanangwe. Hadi kufikia Machi 2026, ujenzi wa kituo cha maonyesho Dimani unaendelea pamoja na matayarisho ya usimamishaji wa nguzo katika ghala la kuhifadhia vifaa, jengo la kuuzia chakula, eneo la kufurahishia watoto pamoja na ukumbi wa mikutano wa kisasa katika kituo cha Dimani.

b) **Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks):** Mradi una lengo la kuimarisha maeneo tengefu ya viwanda ili kurahisisha viwanda vidogo vidogo na vya kati viwe katika maeneo maalum yatakayosaidia kukuza uchumi na kutoa ajira kwa wajasiriamali. Hadi kufikia Machi 2026, kazi ya uandaaji wa Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi, kufanya uchunguzi wa udongo na tathmini ya athari za Mazingira na jamii katika eneo lililotengwa kwa viwanda la Pangatupu. Aidha,

kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji pamoja na ujenzi wa ukuta na jengo la Afisi katika eneo la Chamanangwe.

c) **Programu ya Mageuzi ya Kidigitali:** Programu hii ina lengo la kuimarisha mifumo ya mawasiliano ambayo itarahisisha utoaji wa huduma za kimtandao nchini. Programu itahusisha mifumo mbali mbali Serikalini inayotumika katika utoaji wa huduma zenye ufanisi zaidi za mawasiliano na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2026, kazi zilizofanyika ni pamoja na utoaji wa huduma ya mtandao kwa maeneo ya umma (Public Wi-Fi) katika eneo la Uwanja wa Amani Complex, uwanja mpya wa Fumba, masoko, Forodhani na vituo vya mabasi. Aidha, programu imeendelea na kazi ya uimarishaji wa vifaa kwa kuweka 'Rack' pamoja na '*Rectifier* ' kwa vituo (SITE) vyote Unguja na Pemba.

d) **Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania:** Mradi umeanzishwa kwa lengo la kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula. Hadi kufikia Machi 2026, mafunzo kwa maafisa ugani 400 juu ya namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari, mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji na teknolojia ya kilimo shadidi na mafunzo kwa vijana juu ya kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo yametolewa; pamoja na ununuzi wa vifaa mbali mbali (mashine nne (4) za kupandia mbegu, nne (4) za miche, nne (4) za kupalilia, nane (8) za kuvunia na trekta nne (4) za kufungia mashine za kupandia). Utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa mabwana na mabibi shamba pamoja na wakulima kuhusiana na kilimo himilivu; ufanyaji wa tafiti kwa ajili ya kupata teknolojia zinazohimili mabadiliko ya tabianchi yanaendelea.

e) **Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula:** Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuwa na upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kaya na Taifa kwa ukarabati wa maghala ya

chakula na ujenzi wa vihenge. Hadi kufikia Machi 2026, kazi ya ukarabati wa maghala 8 ya Unguja na Pemba inaendelea. Vile vile, kwa ujenzi wa Kituo cha Uhifadhi wa Chakula – Unguja hatua za manunuzi za kumpata Mshauri Elekezi zimeshaanza na kituo hicho kitakuwa na ukubwa wa G+2 na maabara.

### IV. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

8.0 **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza Programu na Miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 1,243.64 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 746.19 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 432.16 bilioni sawa na asilimia 58 ya lengo la TZS 746.19 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:

a) **Programu ya kuimarisha Miundombinu ya Elimu:** Programu hii ina lengo la kuimarisha Miundombinu ya Sekta ya Elimu ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora yenye viwango na ufanisi. Hadi kufikia Machi 2026, programu imeweza kukamilisha michoro kwa maeneo yatakayojengwa karakana za ufundi ambayo ni Bububu, Mtoni Kigomeni, Abeid Amani Karume, Kwarara, Mwanakwerekwe A, Chumbuni, Forodhani, Hurumzi, Mikunguni, Nyerere, Kwamtipura, Mahonda, Machui, Bambi, Munduli, Langoni na Fuoni kwa Unguja. Pemba ni Vitongoji, Ole, Gando, Wete Sekondari, Kengeja Technical Secondary School, Uweleni, Micheweni na Konde.

Ujenzi wa jengo la Skuli ya Kilimo, Maabara ya Sayansi ya Kisasa, na utoaji wa taaluma ya mahitaji maalum katika Kampasi ya Tunguu unaendelea katika hatua za mwisho pamoja na kuendelea na ujenzi wa dahalia katika Chuo cha Taifa Zanzibar (SUZA). Ukamilishaji wa Chuo cha IIT Madrasa kwa ufungaji wa vifaa vya TEHAMA, kuweka ardhi sawa katika dakhalia pamoja na ujenzi wa uwanja wa mpira. Ujenzi wa karakana za Uhandisi Mitambo, Uhandisi ujenzi, Uhandisi magari katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume unaendelea. Kazi ya kuunganisha Mkonga wa Taifa na skuli, vituo vya ubunifu wa kisayansi (HUBs) na vituo

vya ualimu (TCs) imekamilika, vituo vyote 100 vilivyokusudiwa vimefikiwa na vinapata huduma ya mtandao kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia. Kwa upande wa ujenzi wa jengo la Wizara Chake Chake - Pemba unaendelea katika hatua za umaliziaji na jengo la Unguja unaendelea kwa hatua ya uwekaji wa tofali ghorofa ya nne na upigaji wa plasta. Kwa upande wa Ukarabati na utanuzi wa Kituo cha Habari za Elimu Mkoroshoni – Pemba ujenzi umekamilika na sasa kazi inaendelea kwa Kituo cha Habari za Elimu Kwarara – Unguja.

b) **Programu ya Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo:** Programu ina lengo la kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa. Hadi kufikia Machi 2026, kazi ya ujenzi wa kiwanja kikubwa cha michezo kilichopo Fumba imeanza kwa kuweka nguzo na ujenzi wa majukwaa, usafishaji wa eneo la stadium, *'Ferry pier'*, viwanja vya kufanyia mazoezi, eneo la kuogelea (swimming pool) pamoja na uwekaji ardhi sawa. Kwa upande wa ujenzi wa viwanja 17 vya michezo vya Wilaya na Mikoa viwanja nane vimeshakamilika (Gombani, Maisara, Migombani-Prizi, Kitope, Kitogani, Mombasa, Mwehe na Mao ze Dong) na viwanja tisa (Micheweni, Kangani, Unguja Ukuu, Pangatupu, Pandani, Ukutini, Kinyikani, Matemwe na Maruhubi) ujenzi wake unaendelea katika hatua ya tofauti. Aidha, kwa upande wa ujenzi wa viwanja sita vyenye miundombinu ya michezo ya aina nne katika kiwanja kimoja (4 in 1) Unguja na Pemba viwanja hivi ujenzi wake umekamilika na maeneo yaliyobahatika kujengwa viwanja hivyo ni; Skuli ya Sekondari Tumbatu, Chuo cha Ufundi wa Amali Mkokotoni na Skuli ya Sekondari Regeza Mwendo kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Skuli ya Sekondari Mchanga Mdongo, Skuli ya Sekondari Kangani na Chake Chake. Viwanja hivyo vitahusisha mchezo wa *'Basketball, Netball, Tennis na Volleyball'* kwa kiwanja kimoja.

c) **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Makaazi:** Programu hii ina lengo la kujenga nyumba za kisasa na bora ili kukidhi mahitaji

ya makaazi, hasa katika maeneo yenye ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya nyumba. Programu pia ina lengo la kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati, ili kupunguza changamoto ya uhaba wa makazi. Hadi kufikia Machi 2026, ujenzi wa nyumba za makaazi Chumbuni na Kisakasaka unaendelea. Aidha, Ujenzi wa nyumba za makaazi na biashara zinazojengwa Mkungu Malofa - Chake Chake ujenzi unaendelea katika hatua ya ujenzi wa ghorofa ya kwanza na utiaji plasta chini, kwa Wete na Nyamanzi hatua za awali zinaendelea.

d) **Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja:** Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma zenye kukidhi mahitaji. Hadi kufikia Machi 2026, kazi zinazoendelea ni ubomoaji wa majengo yaliyopo katika maeneo ya mradi na uhamishaji wa vifaa.

e) **Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Binguni:** Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya rufaa na kuimarisha miundombinu ya kufundishia taaluma za Afya. Hadi kufikia Machi 2026, hatua za kumpata Mshauri Elekezi zinaendelea.

### V. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu

9.0 **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 43.3 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 152.19 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 121.25 bilioni sawa na asilimia 80 ya lengo la TZS 152.19 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:

a) **Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama:** Mradi huu una lengo la kuimarisha usalama wa jamii kwa kuhakikisha kuwa kuna miundombinu ya kisasa ya ulinzi na usalama ikiwemo uwekaji wa mifumo na vifaa vya kisasa vya ulinzi ili kulinda wananchi na

mali zao dhidi ya uhalifu na viashiria hatarishi. Hadi kufikia Machi 2026, Mkandarasi ameshakabidhiwa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya CCTV Unguja na Pemba. Kazi ya matengenezo kwa kufanya urejeshaji wa mfumo wa kamera za CCTV inaendelea katika maeneo ya Mji Mkongwe, Michenzani, Kariakoo Mlandege na Biziredi na tayari kamera zimeanza kufanya kazi.

b) **Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa:** Mradi una lengo la kuwa na Mahkama za kisasa zenye mazingira mazuri pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na kuhakikisha upatikanaji wa haki. Hadi kufikia Machi 2026, ujenzi wa Mahkama za Pemba kazi zinaendelea kwa hatua za mwisho ambapo ujenzi wa Mahakama ya Kinyasini - Mkoa wa Kaskazini Changaweni - Mkoa wa Kusini na Konde - Wilaya ya Micheweni umefikia asilimia 88 ya utekelezaji wake. Aidha, samani kwa majengo yote ya Mahakama Unguja na Pemba zimeshanunuliwa na zimeshaanza kutumika.

c) **Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi:** Mradi una lengo la kutathmini na kusaidia kupunguza athari za maeneo yaliyohatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kuchukua hatua mahsusi za kudhibiti na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa pwani. Hadi kufikia Machi 2026, tathmini ya hali halisi ya maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi imefanyika katika maeneo 35 huko Pemba. Tathmini hiyo ilifanyika katika maeneo tofauti kwa shehia tano (5) za Pemba (Kangani, Kukuu, Mjimbini, Kengeja na Kendwa). Miongoni mwa maeneo hayo ni Fufuni, Maweni, Ngezi, Kukuu bandarini, Makunge, Kokoni kubwa na ndogo, Mkunguni, Takawani, Pangani na Chafyani.

## D. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2026

### Malengo na Shabaha za Uchumi Jumuishi kwa Mwaka 2026

**10.0 Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2026 unakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050, Mapitio ya utekelezaji wa

Mpango wa Maendeleo wa mda wa kati ZADEP 2021-2026, Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati unaotarajiwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030.

**11.0 Mheshimiwa Spika**, Kwa takwimu za awali, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 7.5 mwaka 2026 kutoka ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2025 kutokana na sababu zifuatazo:

i Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 9.3 kutoka watalii 917,167 kwa mwaka 2025 hadi watalii 1,002,917 mwaka 2026;

ii Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, Ujenzi wa Mji wa Serikali, Ujenzi wa bandari ya Mangapwani na Mpigaduri na Ujenzi wa Mji wa Michezo Fumba. Miradi mengine itakayochangia ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama, Umeme na Ujenzi wa masoko ya kibiashara;

iii Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili kubakia kwa tarakimu moja;

iv Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali;

v Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza thamani na miradi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;

vi Kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi kutokana na juhudi za Serikali za kukuza uwekezaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira; na

vii Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ya uchumi wa buluu na kuimarisha matumizi endelevu ya Bahari.

**12.0 Mheshimiwa Spika,** Shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2026;

ii. Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja chini ya kiwango cha asilimia 5 kama ilivyo shabaha iliyowekwa kwa nchi za Afrika Mashariki;

iii. Uwiano wa Mapato ya ndani kufikia asilimia 41.4 ya Pato la Taifa mwaka 2026 kutoka asilimia 33.4 mwaka 2025;

iv. Uwiano wa Mapato ya kodi kufikia asilimia 36.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026 kutoka asilimia 33 mwaka 2025;

v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0;

vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi minne; na

vii. Kipato cha mwananchi kuendelea kubakia juu ya wastani wa Dola za Kimarekani 1,449.

**13.0 Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya ukuaji huo yanategemea na misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;

ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;

iii. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu;

iv. Kuwa na uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda ili kuongeza thamani ya bidhaa kwa matumizi ya ndani na usafirishaji nje ya nchi;

v. Kuanza kwa miradi inayotarajiwa kuwa ni nyenzo za kuwezesha Zanzibar kukaribisha timu kwa mazoezi na baadhi ya mechi za Mashindano ya kuwania Kombe la Afrika (AFCON 2027); na

vi. Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama nchini na kwa nchi jirani.

**14.0 Mheshimiwa Spika**, Vile vile, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuweka utulivu wa bei kwa wananchi ikiwemo: -

i. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;

ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei;

iii. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani;

iv. Kuendelea kushajihisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji wa bidhaa za kilimo na za viwandani;

v. Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini; na

vi. Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku hasa kwa vyakula vikuu vinavyolimwa hapa nchini.

**15.0 Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, makadirio ya kasi ya ukuaji wa Uchumi yanaweza kuwa chini ya wastani wa asilimia 7.5 ikiwa mgogoro wa vita baina Marekani-Israel dhidi ya Irani utaendelea kudumu kwa muda mrefu na kupelekea kuathiri baadhi ya shughuli kuu za Uchumi zikiwemo sekta ya utalii, usafirishaji, uwekezaji mitaji na biashara sambamba na kupanda kwa bei za mafuta ambazo zitaathiri uzalishaji wa ndani na uchumi wa dunia kwa ujumla ifikapo mwishoni mwa mwaka 2026.

**16.0 Mheshimiwa Spika,** Kufuatia mwenendo wa sasa wa uchumi wa dunia, hatua madhubuti za sera zinazopendekezwa ili kudhibiti athari hizo na kuimarisha ustahimilivu wa uchumi wa Zanzibar mwaka 2026 zinajikita katika maeneo yafuatayo:

i. **Sera za fedha na bajeti (fiscal policy):** Serikali inapaswa kulenga matumizi yenye tija kubwa, hususan katika miundombinu muhimu, afya, nishati na uzalishaji. Aidha, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani bila kuongeza mzigo mkubwa kwa walipa kodi, pamoja na kuboresha usimamizi wa matumizi ya umma, kutasaidia kudhibiti nakisi ya bajeti na kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali;

ii. **Sera za fedha (monetary policy) na uthabiti wa kifedha:** Kupitia Benki Kuu ya Tanzania, juhudi zielekezwe katika kudhibiti mfumuko wa bei ili ubaki katika tarakimu moja, kusimamia ukwasi (liquidity) kwa uangalifu, na kulinda uthabiti wa sekta ya fedha (financial sector stability). Hatua hizi zitasaidia kupunguza athari za mfumuko wa bei wa bidhaa kutoka nje, hususan nishati na chakula. Serikali inapaswa kuimarisha usimamizi wa bei za bidhaa muhimu na kuanzisha akiba ya kimkakati ya chakula na nishati ili kukabiliana na athari za mtikisiko wa uchumi wa dunia, kupunguza utegemezi na matumizi ya fedha za kigeni katika miamala ya ndani na kuimarisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa za msingi ili kupunguza utegemezi wa uagizaji na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya bei za bidhaa kutoka nje ya nchi katika uchumi wa Zanzibar;

iii. **Usimamizi wa sekta ya nje (external sector management)**: Kuimarisha mapato ya fedha za kigeni kupitia sekta ya utalii, mauzo ya bidhaa nje ya nchi ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, mazao ya baharini na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (Foreign Direct Investment). Pia, juhudi za kubadili vyanzo vya nishati na kuongeza matumizi ya nishati mbadala zitasaidia kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya bei za bidhaa hiyo;

iv. **Kuimarisha sekta za uzalishaji wa ndani:** Kuwekeza zaidi katika kilimo, uvuvi, viwanda vidogo na vya kati pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa (value addition). Hatua hizi zitapunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuongeza ajira pamoja na mapato ya ndani;

v. **Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji:** Kuendelea kurahisisha taratibu za uwekezaji, kupunguza urasimu, na kuimarisha miundombinu ya biashara na huduma. Hii itasaidia kuvutia wawekezaji zaidi na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi ambayo ni msingi muhimu wa Uchumi; na

vi. **Kuimarisha mifumo ya ulinzi wa jamii (social protection):** Kusimamia mifumo ya kusaidia kaya zilizo katika mazingira magumu dhidi ya athari za mfumuko wa bei, hususan kwa bidhaa muhimu za chakula. Hii itasaidia kulinda ustawi wa wananchi na kudumisha utulivu wa kijamii na kiuchumi (maintain social and economic stability).

**17.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla, utekelezaji madhubuti wa sera hizi utawezesha Zanzibar kupunguza athari za mishtuko ya nje (external shocks), kuimarisha udhibiti wa uchumi, na kulinda matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2026 licha ya changamoto za Kimataifa zinazoendelea.

## E. MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/2027

**18.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2026/2027, Mpango wa Maendeleo utazingatia zaidi utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayolenga kukuza uchumi, kuimarisha huduma za jamii, kuongeza mapato ya Serikali, kukuza ajira na kuimarisha ulinzi na usalama. Lengo ni kuleta matokeo ya haraka katika kufikia maendeleo ya nchi na kuinua hali za wananchi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Miongoni mwa vipaumbele ni kukamilisha utekelezaji wa miradi muhimu kwa ajili ya kufanikisha mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) kwa ufanisi na viwango vya Kimataifa, pamoja na kuendelea na miradi iliyoanzishwa miaka ya nyuma ambayo bado haijakamilika.

**19.0Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027 utazingatia misingi ya utawala bora, matumizi bora ya fedha (value for money), ufuatilaiji na tathmini ili kuhakikisha malengo yanayotarajiwa yanafikiwa.

## F. Mapendekezo ya Maeneo ya Kimkakati kwa Mwaka 2026/2027

**36.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na Mkakati wa kuibadilisha Taswira ya Zanzibar kwa kuweka mbele maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia maeneo manne ya Kimkakati kama yalivyoainishwa katika Dira na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar ambayo ni: **(i) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; (ii) Kuimarisha Miundombinu Wezeshi; (iii) Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii na (vi) Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu**. Kwa mwaka 2026/2027, Mpango wa Maendeleo umepanga kutumia kiasi cha TZS 3,920.59 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi ya kimkakati sawa na ongezeko la asilimia 19.1 ikilinganishwa na TZS 3,292.22 bilioni za Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2025/26. Programu na miradi itakayotekelezwa katika maeneo hayo italenga kufikia yafuatayo:

### I. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

**20.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na utekelezaji wa sera na mikakati ya kuendeleza miundombinu ya bahari kuu, viwanda vya kusarifu mazao ya baharini, na utalii wa bahari na visiwa. Kuimarisha kilimo cha biashara na usalama wa chakula na kuwezesha upatikanaji wa ajira za Serikali na Sekta Binafsi. Jumla ya TZS 669.94 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kugharamia programu na miradi katika eneo hili.

### II.Kuimarisha Miundombinu Wezeshi

**21.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu wezeshi ya usafiri wa anga, baharini na nchi kavu, kuimarisha uwezo wa Zanzibar katika nishati ya umeme na kuendeleza miundombinu ya uzalishaji, usambazaji na uunganishaji wa umeme. Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama, kuongeza ubora wa matumizi ya TEHAMA na huduma za kidijitali na kuendeleza makaazi yanayozingatia muundo na haiba za miji. Jumla ya TZS 1,757.74 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kugharamia programu na miradi katika eneo hili.

### III. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

**22.0 Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu na huduma za afya, elimu, michezo pamoja na mifumo ya hifadhi ya jamii. Jumla ya TZS 1,275.96 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kugharamia Programu na Miradi katika eneo hili.

### IV.Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu

**23.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kuimarisha upatikanaji wa haki ili kuhakikisha nchi inaendelea kubaki katika hali ya utulivu na amani sambamba na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Jumla ya TZS 216.95 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kugharamia Programu na Miradi katika eneo hili.

## Rasilimali kwa Ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2026/2027

**37.0 Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha TZS 5,779.15 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Programu 38 na Miradi 54 ya Maendeleo. Fedha hiyo ni sawa ongezeko la asilimia 27.30 ya makadirio ya bajeti ya maendeleo yam waka 2025/2026 ya TZS 4,539.64 bilioni. Kati ya fedha hizo (TZS 5,779.15 bilioni), TZS 4,433.80 bilioni sawa na asilimia 76.72 ya bajeti ya maendeleo ni kutoka mapato ya ndani na TZS 1,345.35 bilioni (TZS 240.10 bilioni ni ruzuku na TZS 1,105.25 bilioni na mkopo) sawa na asilimia 23.28 ya bajeti ya maendeleo ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**38.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa mwaka 2026/2027, imepanga kutumia kiasi cha 3,797.39 bilioni sawa na asilimia 65.71 kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati na TZS 1,381.76 bilioni kwa miradi mengineyo ikiwemo miradi iliyokuwa haijakamilika kwa mwaka 2025/2026 na miradi ambayo Serikali ina dhima “Commitment” ya kuchangia miradi hiyo kwa mujibu wa makubaliano na Washirika wa Maendeleo wanaochangia katika utekelezaji wa miradi hiyo pamoja

na TZS 600.00 bilioni kwa ajili ya Mfuko wa Ulipaji wa Madeni kwa Miradi ya Maendeleo.

## G. MAENEO MTAMBUKA

### Masuala ya Idadi ya Watu

**24.0 Mheshimiwa Spika,** Idadi ya watu Zanzibar ni yenye kuongezeka kila mwaka ambapo panahitajika kuwa na takwimu sahihi ili kuweza kupanga mipango sahihi ya maendeleo. Kwa mujibu wa Makadirio ya Taifa ya Idadi ya Watu (National Population Projection) ya mwaka 2023, Zanzibar kwa mwaka 2026 inakadiriwa kuwa na jumla ya idadi ya watu 2,161,086 (wanaume ni 1,052,940 na wanawake ni 1,108,146). Vile vile kasi ya ukuaji wa Idadi ya watu inakadiriwa kuwa ni asilimia 2.9 kwa mwaka. Aidha, kiwango cha watu wanaoishi katika eneo husika kwa kila kilomita ya mraba (population density) kimeongezeka kutoka watu 530 mwaka 2012 hadi watu 768 kwa mwaka 2022.

**25.0 Mheshimiwa Spika,** Katika kuzingatia takwimu hizo na athari zake, Serikali kupitia Tume ya Mipango imekuwa ikifanya jitihada tofauti katika kuimarisha masuala ya idadi ya watu ikiwemo kukamilisha Sera ya Idadi ya Watu ili kupatikana kwa muongozo kamili; Kuanzisha utaratibu wa kuwajengea uwezo Maafisa Mipango wa Taasisi za Serikali na binafsi juu ya kuoanisha viashiria vya masuala ya idadi ya watu katika mipango na bajeti. Aidha, ripoti mbili za masuala ya idadi ya watu zimeandaliwa zenye kichwa cha habari "Uhusiano wa Ukuaji wa Idadi ya Watu, Mabadiliko ya Tabianchi na Upatikanaji wa Huduma za Afya" na "Fursa ya Kukuza Uchumi Miaka Ijayo Kupitia Idadi ya Watu Iliyopo Sasa" ambapo mapendekezo ya ripoti hizi yatatumika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa.

**26.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2026/2027, Tume ya Mipango imejipanga kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Mgawanyo wa Idadi ya Watu na faida zake (Zanzibar Demographic Dividend Implementation Plan); Kuendelea Kuingiza taarifa za kaya na majengo katika mfumo wa shehia pamoja na kuunganisha Mfumo wa Usajili wa Taarifa za

Shehia (Shehia Register) na mifumo mengine ili kuweza kusomana na kupata taarifa sahihi; na Kufanya uzinduzi wa Sera ya Idadi ya Watu Zanzibar.

**Taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi**

**27.0 Mheshimiwa Spika,** Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (HBS) ni chanzo kikuu cha kutoa viashiria vya upimaji na utekelezaji wa jitihada za Serikali katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini. Matokeo ya awali, utafiti huu unaonesha kuwa, kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Zanzibar umeendelea kushuka kutoka asilimia 34.4 mwaka 2009/2010, asilimia 30.4 mwaka 2014/2015, asilimia 25.7 mwaka 2019/20 hadi asilimia 19.9 mwaka 2025. Hali ya Umaskini wa mahitaji ya msingi maeneo ya mijini umepungua na kufikia asilimia 14.8 kutoka asilimia 15.5 mwaka 2019/2020. Kwa upande wa maeneo ya vijijini, hali ya umaskini umepungua na kufikia asilimia 24.8 kutoka asilimia 33.7 mwaka 2019/20.

**28.0 Mheshimiwa Spika,** Hali ya umasikini usio wa kipato (non-monitoring poverty) kwa Zanzibar, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kaya zinaendelea kuimarika kwa kujenga nyumba bora ambazo zinatumia vifaa vilivyo bora vya ujenzi (paa, sakafu na ukuta). Matokeo yanaonesha kuwa kaya zinazotumia mapaa yaliyo bora yameongezeka hadi kufikia asilimia 96 mwaka 2025 kutoa asilimia 91.3 mwaka 2019/2020, kaya zinazoishi katika nyumba zenye kuta imara zimeongezeka hadi kufikia asimia 89.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 82.3 mwaka 2019/2020, aidha, kaya zenye sakafu imara zimeongezeka hadi kufikia asilimia 91.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 82.7 mwaka 2019/2020.

**Uhifadhi wa Mazingira**

**29.0 Mheshimiwa Spika,** Katika kulinda na kuhifadhi mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kwa mwaka 2025/2026, Serikali ilifanikiwa kufanya mambo tofauti yakiwemo: Kutoa elimu, miongozo na ushauri juu ya uhifadhi na utunzaji wa Mazingira na Mabadiliko

ya Tabianchi kupitia maonesho na vipindi vya Redio; Matayarisho ya ujenzi wa hodhi la kuvunia maji ya mvua lenye uwezo wa kuhifadhi lita za ujazo 9,000 huko Bumbwini Mafufuni yamekamilika na ujenzi utaanza mara baada ya kupatikana kwa mkandarasi wa ujenzi; Kutoa mafunzo na kushiriki katika mikutano na warsha mbalimbali nchini yenye malengo tofauti ikiwemo biashara ya hewa ya kaboni, mpango wa matumizi ya bahari na bioanuai. Kushirki katika mikutano mbali mbali ya kikanda na Kimataifa; Kutekeleza programu ya kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wenye lengo la kuzijengea uwezo Taasisi za Kitaifa na katika ngazi ya Jamii, Kufanya uwekezaji wa miradi ya kimazingira na mabadiliko ya tabianchi ndani ya jamii; na Kutekeleza Programu Jumuishi ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira Zanzibar (ZJP) kwa kushirikiana na Washirika mbalimbali wa Maendeleo.

**30.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali katika mwaka 2026/2027 imepanga Kutayarisha Kanuni na Miongozo ya Kimazingira; Kufanya tathmini ya mmong'onyoko wa ardhi Unguja; Kukuza uelewa kwa jamii juu ya maswala ya mazingira na Mabadiliko Tabianchi; Ujenzi wa miundombinu himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya fukwe ili kuzuia maji ya bahari kuingia katika maeneo ya kilimo na makaazi; Kuziwezesha Serikali za Mitaa 11 kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na Kutekeleza ujenzi wa mradi wa mazingira na utalii katika eneo la Tibirinzi – Chake Chake Pemba.

**Makundi yenye Mahitaji Maalum**

**31.0 Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu limekamilisha uandaaji wa Rasimu ya awali ya Muongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar; Elimu kwa umma juu ya haki za watu wenye ulemavu imetolewa katika ushiriki na ushirikishwaji; Ukaguzi wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu kwa majengo kumi ya umma kupitia Wizara tano za Serikali kwa upande wa Pemba; na Kuandaliwa kwa Mpango Mkakati wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu wa miaka mitano ijayo kuanzia 2026 hadi 2030.

**32.0 Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Taasisi ya Qatar Charity Organization, Emarate Leasure, All about albinisim, limefanikiwa kuratibu upatikanaji wa jumla ya vifaa saidizi 773 (Motor Wheelchair 60, Sun screen 377, kofia 236 na miwani 100). Vile vile, katika kuunga mkono jitihada za watu wenye ulemavu, baraza limesimamia upatikanaji wa vyarahani 110, vitambaa 350, nyuzi boksi 200, mikasi 50, zipu 1,250, meza 50, viti 50 na visanduku 50.

**33.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2026/2027 Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu limejipanga zaidi ujumuishaji wa Watu wenye Ulemavu, Uwezeshaji wa Watu wenye Ulemavu, Kukuza uelewa wa jamii juu ya masuala ya Watu wenye Ulemavu, na Kuimarisha huduma za Afisi.

**Kudhibiti Madawa ya Kulevya**

**34.0 Mheshimiwa Spika**, Dawa za kulevya bado ni miongoni mwa masuala mtambuka yanayohitaji mazingatio maalum. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imeendelea na juhudi mbali mbali za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya Zanzibar. Kwa kipindi cha mwaka 2025/2026, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imeweza kutekeleza yafuatayo: Kufanya Operesheni za kuwakamata wahalifu wa dawa za kulevya ambapo kupitia operesheni hizo jumla ya watuhumiwa 199 (Wanaume 177 na Wanawake 23) wa dawa za kulevya walikamatwa; Kufungua kesi za dawa za kulevya ambapo jumla ya  kesi 164 (136 Unguja, 28 Pemba) zilifunguliwa; Kuwafikisha watuhumiwa wa kesi za dawa za kulevya kupitia vyombo vya sheria na kuwafungulia kesi Mahakamani ambapo kesi 40 (Unguja 29, Pemba 15) zimetolewa hukumu kati ya hizo, kesi 24 zimeachiliwa huru na kesi 20 zimepata hatia na kesi 201 bado zinaendelea Mahakamani; Vile vile mali zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni moja nukta moja (1,135,800,000/=) zimetaifishwa; na Kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya pamoja na Sheria Nambari 8 ya 2021 katika maeneo mbali mbali ikiwemo Taasisi za Elimu, Masheha, Wananchi, Vikosi vya Ulinzi na Usalama na maeneo ya kazi kwa Unguja na

Pemba ambapo jumla ya watu waliofikiwa na taaluma hizo ni 23,693 (wanaume 11,741 na wanawake 11,952).

**35.0 Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2026/2027, Afisi imejipanga kuendelea kufanya Operesheni kubwa na za kawaida katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba; na Kuendelea kutoa taaluma na hamasa kwa jamii kuhusiana na masula ya dawa za kulevya, masuala ya VVU/UKIMWI, Masuala ya watu wenye Ulemavu na masuala yanahusiana kutunza na kuhifadhi mazingira.

**Mipango ya Kuendeleza Watenda Kazi**

**36.0 Mheshimiwa Spika,** Taaluma na ujuzi ni vitu muhimu ambavyo watu wamewekeza katika maisha yao na kuwezesha kuwa miongoni mwa wazalishaji wabobezi katika jamii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuimarisha masuala ya rasilimali watu ili kuleta tija na manufaa katika jamii. Katika kufanikisha hilo, Tume ya Mipango ilishirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya Zanzibar kutoa muongozo wa vipaumbele vya elimu vya Taifa utakaowasaidia wanafunzi kupata mikopo ya elimu ya juu; kutoa uwelewa kwa wanafunzi wa skuli za sekondari juu ya fani za kipaumbele; Kuandaliwa kwa Muongozo wa kufanya mazoezi ya vitendo kazini (Zanzibar Internship Guildelines); na Kuandaliwa kwa Mfumo wa Rasilimali Watu Zanzibar (Zanzibar Human Capital Platform).

**37.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2026/2027, Tume ya Mipango inakusudia kuzindua Sera ya Maendeleo ya Rasilimali Watu Zanzibar; Kuunganisha Mfumo wa Rasilimali watu Zanzibar na mifumo mingine ili kubadilishana taarifa na kuongeza ufanisi; Kuendelea kutoa uwelewa kwa wanafunzi wa skuli za sekondari juu ya fani za kipaumbele; Kutayarisha ripoti ya hali ya ujuzi Zanzibar; na Kutayarisha Mkakati wa Rasilimali Watu wa Zanzibar (Zanzibar Human Capital Strategic Plan).

## H. UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI

**38.0 Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2026/2027, Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar imepanga kusimamia na kufuatilia pamoja na kufanya Tathmini ya Mpango wa Maendeleo kama ifuatavyo:-

i. Kuandaa na kuchapisha Mapitio ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 kwa kipindi cha miaka 5 (2021-2026);

ii. Kutoa uwelewa kwa Wizara, Idara, Taasisi zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, Taasisi Binafsi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na Asasi za Kiraia juu ya matumizi ya Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Zanzibar ya mwaka 2026;

iii. Kuandaa na kuchapisha ripoti ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo (ZADEP 2021-2026);

iv. Kufanya Tathmini ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo iliyokamilika na inayoendelea;

v. Kuandaa na kuchapisha , miogozo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E framework na M&E guideline)

vi. Kuandaa Mkakati wa Mawasiliano wa kupata taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini;

vii. Kuandaa na Kuchapisha Ripoti ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa Zanzibar kwa mwaka 2026–2027; na

viii. Kuandaa na kuchapisha ripoti ya Hiari ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (Voluntary Local Review) kwa ngazi ya Mikoa kwa mwaka 2026/2027.

## I. MAJUMUISHO

**39.0 Mheshimiwa Spika,** Utekekezaji wa Mpango wa mwaka 2026/2027 unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa kuimarisha utulivu wa viashiria vya uchumi na kasi ya ukuaji wa uchumi. Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani hususan kwa

kutumia mali ghafi za kilimo na uvuvi; kuongeza uwekezaji katika maeneo mbali mbali ikiwemo visiwa vidogo vidogo na katika maeneo huru ya kiuchumi; kuendeleza ujenzi wa miundombinu wezeshi na kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji.

**40.0 Mheshimiwa Spika,** Uwasilishaji huu usingewezekana leo hii bila ya mchango mkubwa wa maelekezo, miongozo na mawazo ya wadau mbalimbali, Serikalini na katika Sekta Binafsi. Kwa ujumla wao, naomba uniruhusu niwashukuru sana wote kwa namna walivyosaidia na kufanikisha mimi leo hii kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba kwa dhamana niliyopewa ya Uwaziri wa Fedha na Mipango. Naomba uniruhusu niwataje wachache.

**41.0 Mheshimiwa Spika,** Kwanza naomba nishukuru sana maelekezo na miongozo ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Dira na upeo wa kuona mbali kwa Mheshimiwa Rais, na utayari wake wa kutuongoza bila ya kinyongo na khiana na uzoefu wake mkubwa katika uongozi wa Serikali ni faraja kubwa kwetu sote na kwangu mimi binafsi. Kwa kauli hiyo hiyo, namshukuru sana msaididzi wake mkuu, Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla nae kwa kutusimamia na kutuelekeza bila ya kuchoka, tunajifunza mengi kutoka kwao muda wote.

**42.0 Mheshimiwa Spika,** Pili ni wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Wenyeviti tunaelewa kazi ngumu ya kuliongoza Baraza hili. Uweledi wenu umesaidia sana kuleta utulivu wa Baraza kwa kusimamia wananchi wakiwakilishwa vyema na Wawakilishi wao, ambao wanaisimamia vyema Serikali katika kuwajibika kwa wananchi kupitia chombo hichi adhimu. Hakika hii si kazi nyepesi lakini mnaimudu na kuitekeleza vyema.

**43.0 Mheshimiwa Spika,** Tatu naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir (Mrembo) na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Baraza lako hili. Tunapata na kuthamini sana mashirikiano makubwa kutoka Kamati na Mwenyekiti wake.

Miongozo na michango yao siku zote inaibua fikra mpya na za kimaendeleo na tumekuwa tukiipokea na kuifanyia kazi kwa dhati. Tunafanya kazi na Kamati hii kwa maelewano yasioathiri majukumu ya kila upande.

44.0 **Mheshimiwa Spika,** Nne naomba kuwashukuru kwa dhati Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti na watendaji wote walioshiriki katika maandalizi ya Mpango huu. Michango na upeo wao umesaidia sana kuyaweka sawa makadirio haya na hivyo kuwezesha kuwasilishwa Barazani leo hii.

45.0 **Mheshimiwa Spika,** pamoja na wote hao, kazi kubwa ya uandaaji wa Mpango wa Maendeleo huu imefanywa na Tume ya Mipango. Nathamini na kushukuru sana uongozi na msaada mkubwa wa Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dr. Afua Khalfan Mohamed na Niwashukuru pia Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango CPA Aboud Hassan, Mhasibu Mkuu, CPA Hamad Saleh Hamad kwa kufanya kazi kwa karibu na Tume ya Mipango. Vile Vile, nawashukuru Makamishna wote akiwemo Ndugu Mohamed Msoud Salim - Kamishna na Idara ya Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Kisekta, Dkt. Zuhura Mohamed Abdalla - Kamishna Idara ya Ufuatiliaji na Tathmin, Dkt. Ameir Sheha Haji - Kamishna Idara ya Ukuzaji Uchumi na Dkt. Rukkaiya Wakif Mohamed - Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Watendakazi pamoja na watendaji wengine walioshiriki kwa namna moja au nyengine katika kufanikisha hotuba hii. Haya ndio mafanikio mengine makubwa yanayopatikana katika kufanya kazi kwa mashirikiano ambayo yanapaswa kudumishwa ili kuweza kufanikisha malengo ya Kitaifa.

46.0 **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kushirikiana na Mataifa na Mashirika mbali mbali. Kwa namna moja au nyengine, mashirikiano hayo yamesaidia sana katika kuharakisha maendeleo yetu. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, natoa shukran za dhati kwa Mataifa na Mashirika hayo. Naomba niwatambue Washirika wa Maendeleo wa ndani kwa mwaka 2026/2027 kama ifuatavyo: PBZ, ZSSF, ZANZIBAR MILELE FOUNDATION, ZANZIBAR MAISHA BORA FUNDATION, MWANAMKE INITIATIVE FOUNDATION, NMB,

NBC, CRDB na COSTECH. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo wa nje na nchi rafiki zinazoendelea kushirikiana nasi kwa mwaka 2025/2026 ni pamoja na ACRA, AF, AFD-FRANCE, AfDB, ALSF, AMREF, AUSTRIA, BADEA, BELGIUM, CHINA, (CIDA) CANADA, DANIDA, DfID, DLI-GPE, EDF, EDCF, ENABEL, EU, EXIM BANKS za India, China na Korea, FAO, FCDO, FINLAND, GATE FOUNDATION, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, GERMANY (GIZ AND KfW), GPE, GOOD NEIGHBOURHOOD, HIPZ, IAEA, INDIA, IFAD, ILO, IMF, IRELAND, JAPAN (JICA), KHALIFA FUND, MFUKO WA MAENDELEO WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE), KOICA, KOREA (KRC), KUWAIT FUND, LAD, MALAYSIA, NETHERLAND, NORWAY/NORAD, OMAN, OPEC FUND, PHARM ACCESS INTERNATIONAL, PMI, QATAR CHARITY ORGANISATION, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, STBF, SULTANATE OF OMAN, SWEDEN, THPS, TfT, UK, UKEF/CITI BANK NA DEUTCH BANK, UN, UNCDF, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, UNICREDIT BANK, UNIDO, USAID, UN WOMEN, UTURUKI, VITAL STRATEGIES, WORLD BANK na WHO. Kipekee naomba nitoe shukrani kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushirikiana na Zanzibar katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

## J. HITIMISHO

**47.0 Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii na vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2025 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/2026 na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2026 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027 ambavyo vina taarifa na uchambuzi wa kina vinapatikana pia katika tovuti ya Tume ya Mipango (http://planningznz.go.tz).

**48.0 Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa Baraza hili lipokee na kujadili Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2026 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2026/2027 wenye kugharimu kiasi cha **TZS 5,779.15 bilioni.**

**49.0 Mheshimiwa Spika,** kwa heshima naomba kutoa hoja.

Dkt. Juma Malik Akil (*MBM*)
**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**